HOTUBA YA MTENDAJI MKUU KATIKA MAADHIMISHO YA SIKU YA USALAMA NA AFYA MAHALI PA KAZI DUNIANI, TAREHE 28 APRILI, 2022

VIWANJA VYA UKUMBI WA JAKAYA KIKWETE

Mheshimiwa Prof. Joyce Ndalichako (MB), Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu na waalikwa wote mliojumuika nasi hapa.

Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania….

Mheshimiwa Mgeni Rasmi; awali ya yote napenda kumshukuru Mungu Mwingi wa Rehma kwa kutujalia afya njema na kwa kibali na neema yake imempendeza kutukutanisha hapa leo kwenye kilele cha maadhimisho ya siku hii ya usalama na afya mahali pa kazi duniani.

Pili, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kukubali mwaliko wetu wa kuwa Mgeni Rasmi pamoja na majukumu mazito uliyonayo hasa katika kipindi hiki cha bunge, lakini Kwa kutambua na kuthamini shughuli hii, umekubali kuwa nasi leo katika maadhimisho haya, nakushukuru sana na karibu sana.

Vilevile, naomba niwashukuru wadau wetu wa utatu, TUCTA na ATE bila kuwasahau Shirika la Kazi Duniani (ILO) kwa kushirikiana nasi bega kwa bega katika maandalizi ya maadhimisho haya, kwa kipekee kabisa naomba nimshukuru Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Kazi Duniani Kanda ya Afrika Mashariki, Bwana Wellington Chibebe kwa namna ambavyo amekuwa akishirikiana na Taasisi yetu katika kutekeleza miradi mbalimbali na ambayo imekuwa ikifanikiwa sana.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi; pamoja na shukrani hizo, kazi yangu hapa ni kukutambulisha wageni mbali mbali waliopata fursa ya kujumuika nasi katika maadhimisho haya yanayofanyika kitaifa hapa jijini Dodoma na kwa heshima na taadhima, naomba utambue uwepo wa wageni wafuatao;

Mheshimiwa, George Simbachawene (MB), Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera,Uratibu na Bunge,

Mheshimiwa, Patrobas Katambi (MB), Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu- Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu**,**

Mheshimiwa, Ummy Nderiananga, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu-Sera, Uratibu na Bunge,

Mh. Antony Mtaka, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma,

Mhe. Jabir Shekimweli - Mkuu wa Wilaya Dodoma Mjini,

Prof. Jamal Katundu, Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu- Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu,

Dr. John Jingu, Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu- Sera, Bunge na Uratibu,

Ndugu Kaspar Kaspar Mmuya, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu- Sera, Bunge na Uratibu.

Mheshiwa, Dkt. Joseph Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Katiba na Sheria ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (MB), Makamu Mwenyekiti Kamati ya Kudumu ya Katiba na Sheria ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria waliopo hapa ambao ni pamoja na;

- Mhe. Joseph Tadayo (Mb);
- Mhe. Zainab Katimba (Mb);
- Mhe. Khadija Taya (Mb) na;
- Mhe. Edward Ole Kaita (Mb)

Dkt. Adelhem Meru, Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya OSHA (MAB).

Bi. Getrude Sima, Mwakilishi kutoka Shirika la Kazi Duniani Ofisi ya Tanzania.

Bi. Suzanne Ndomba-Doran, Mkurugenzi Mkuu wa Chama cha Waajiri Tanzania ATE.

Tumaini Nyamhokya, Rais wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Nchini.

Ndugu Hery Mkunda, Katibu Mkuu Shirikisho la Vyama Vya Wafanyakazi Nchini.

Bi. Suzan Mkangwa, Kamishna wa Kazi

Dkt. John Mduma, Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi.

Ndugu Masha Mshomba, Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii- NSSF.

CPA. Hosea Kashimba, Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma,

Wakurugenzi wote mliopo hapa, kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana Ajira na Wenye Ulemavu,

Wakurugenzi kutoka Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA).

Watendaji wote wa Serikali mliopo hapa,

Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi, wakiwemo Wenyeviti na Makatibu Wakuu wa mikoa,

Wakuu wa Taasisi mbali mbali,

Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Dodoma,

Washiriki wote wa maadhimisho haya,

Waandishi wa Habari,

Mabibi na Mabwana.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi, hawa ni baadhi ya viongozi walioweza kufika hapa kushirikiana nasi katika maadhimisho haya ya siku ya Usalama na Afya Duniani. Nami kwa niaba menejimenti na watumishi wa OSHA naomba niseme KARIBUNI SANA.

Pamoja na kazi hii muhimu ya kukutambulisha wageni tulioungana nao leo, kwa idhini yako naomba nitumie fursa hii kueleza kwa kifupi chimbuko la maadhimisho haya na shughuli mbalimbali ambazo tumezifanya ikiwa ni mojawapo ya kampeni za kuhamasisha umuhimu wa kuzingatia masuala usalama na afya mahali pa kazi.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi: Tanzania leo inaungana na mataifa mengine duniani kuadhimisha siku ya afya na usalama mahali pa kazi, maadhimisho haya ambayo hufanyika kila mwaka, huandaliwa na OSHA kwa niaba ya Serikali kwa kushirikiana na wadau wa utatu (tripartite) ambao ni Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi (TUCTA), Chama cha Waajiri Tanzania (ATE) pamoja na Shirika la Kazi Duniani (ILO) ambapo kupitia vikao mbalimbali hujadili namna ya kuiadhimisha siku hii ambapo ujumbe wa mwaka huu uliotolewa na Shirika la Kazi Duniani ni: **Kwa pamoja tushirikiane kujenga utamaduni bora wa Usalama na Afya mahali pa kazi.**

Mhe. Mgeni Rasmi; Chimbuko la Maadhimisho haya yalianza kwa mara ya kwanza Aprili 28, 1996 katika Jiji la New York nchini Marekani na yalikuwa yakiadhimishwa kila mwaka na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Duniani chini ya ufadhili wa Shirika la Maendeleo Endelevu la Umoja wa-Mataifa. Lengo kubwa la maadhimisho haya ilikuwa ni kuwakumbuka wafanyakazi waliokuwa wanaumia, kuugua, kupata ulemavu au kupoteza maisha wakiwa wanatekeleza majukumu yao. Ilipofika mwaka 2003, Shirika la Kazi Duniani (ILO) likaungana na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi

katika kuadhimisha siku hiyo. Mwaka uliofuata yaani 2004, ILO likapendekeza kuwa lengo la maadhimisho hayo libadilike. Badala ya kuadhimisha kwa kusikitika, kuhuzunika, kuwasha mishumaa, kuweka maua na maandamo, ikapendekezwa kuwa maadhimisho hayo yafanyike kwa kuhamasisha wafanyakazi, waajiri na umma kwa ujumla kufanya juhudi za makusudi kabisa ili kuzuia ajali, magonjwa na vifo miongoni mwa wafanyakazi. Kuanzia wakati huo, kila mwaka ILO kwa kushirikiana na wadau wa utatu wamekuwa wakitoa kauli mbiu tofauti tofauti zenye lengo la kuimarisha Usalama na Afya sehemu za kazi na kuziomba nchi wanachama waanze rasmi kuadhimisha maadhimisho haya. Hapa kwetu Tanzania tumekuwa tunafanya maadhimisho haya kwa takribani miaka 18 sasa.

Mhe. Mgeni Rasmi; napenda nikiri kwamba lengo la kubadili dhana ya maadhimisho kutoka kwenye vilio na masikitiko ya wafanyakazi hadi kwenye kampeni mbali mbali za kuelimisha na kuhamasisha uzingatiaji wa masuala ya Usalama na Afya katika sehemu za kazi, limekuwa na matokeo chanya kwani kumekuwa na mwamko na mwitikio mkubwa sana kutoka kwa waajiri, wafanyakazi na umma kwa ujumla kuhusiana na dhana ya maadhimisho haya.

Mhe. Mgeni Rasmi; masuala ya Afya na Usalama ni masuala mtambuka, yanagusa sekta zote za uchumi na kwamba pamoja na kuwa ni takwa la kisheria, lakini kwasasa masuala haya yanaangaliwa zaidi katika mlengo wa haki za binadamu, na kiutu zaidi, kwa mantiki hiyo elimu na ushirikishwaji wa pande zote za utatu ni muhimu sana ili kufikia azma ya lengo la nane (8) la Maendeleo Endelevu ya Dunia (Sustainable Development Goals) linalotaka kuwe na maendeleo ya ukuaji wa uchumi unaozingatia ajira zenye staha kwa watu wote.

Mhe. Mgeni Rasmi; nieleze kwa kifupi hali ya Usalama na Afya ilivyo kidunia ambapo takwimu zinaonesha kuwa ni janga la kiuchumi na kijamii na endapo

hapatakuwa na jitihada za makusudi za kuwekeza katika mifumo thabiti ya kumlinda mfayakazi ambaye ndio nyenzo kuu katika uzalishaji mali, maisha ya wafanyakazi yataendelea kuwa duni siku hadi siku.

Mhe. Mgeni Rasmi; inasikitisha kuona kwamba kumekuwa na ongezeko la ajali, magonjwa na vifo vitokanavyo na kazi kila mwaka ambapo licha ya ajali hizi na magonjwa kuleta madhila kwa wahusika, huleta pia msongo kwa jamii inayohusika. Madhila haya hayapo tu kwenye jamii lakini sehemu za kazi nazo zimekuwa zikipata hasara kutokana na; kwanza kumpoteza mfanyakazi na wafanyakazi kutokuwepo kazini kwa kipindi fulani yaani (absence from work) na kuendelea kulipa mishahara wakati mfanyakazi akiwa mgonjwa, kupoteza taswira ya biashara, kuingia kwenye migogoro ya kisheria, uhabiribu wa mali pamoja na kuingia gharama za mafunzo kwa wafanyakazi wapya.

Kimsingi, gharama za matokeo yote haya ya kibinadamu na uchumi yanayotokana na kukoseka kwa mifumo thabiti ya afya na usalama katika sehemu za kazi, yanapelekea kudorora kwa shughuli za uzalishaji na hivyo kuathiri uchumi wa nchi yetu na dunia kwa ujumla. Hivyo ni wakati mwafaka sasa kwa wadau kukaa na kujadili namna ya kuweka mifumo ya kulinda nguvukazi ya taifa na kutoa kipaumbele katika kumlinda mfanyakazi. Jambo hili litawezekana endapo tutaondokana na dhana ya kwamba masuala ya afya na usalama yanaongeza gharama za uendeshaji na uzalishaji na ndio maana ujumbe wa mwaka huu umejikita katika kuhamasisha uwepo wa ushirikiano baina ya wadau wote katika kujenga utamaduni bora wa afya na usalama mahali pa kazi.

Mhe. Mgeni Rasmi; hivyo kampeni ya mwaka huu imejikita zaidi katika kuhakikisha kuwa kunakuwa na ushirikishwaji katika ngazi zote za maamuzi wakiwemo wafanyakazi ili nao wawe sehemu ya maamuzi na hivyo kujenga utamaduni wa kukinga zaidi kuliko kusubiri mambo yaharibike ndipo hatua

za kuyarekebisha zichukuliwe. Utamaduni huu ukijengeka utapelekea kupunguza ajali, magojwa na vifo vinavyotokana na mazingira hatarishi ya kazi na hivyo kuongeza tija katika uzalishaji ndani ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi; katika kutekeleza hayo yote kwa mwaka huu wadau, wameazimia kutekeleza shughuli mbali mbali zinazolenga kuhamasisha utekelezaji wa **Sheria Na.5 ya Mwaka 2003 ya Usalama na Afya mahali pa kazi** kwa kufanya yafuatayo:

- Kuendelea kufanya kaguzi za kiusalama na kiafya katika sehemu kazi ikiwemo ofisi za serikali, Taasisi za umma na kukagua miradi ya kimkakati na kushauri ipasavyo.

- Kufanya mafunzo mbalimbali ya utekelezaji wa sheria tajwa, kama vile uundaji na usimamizi wa kamati za Usalama na afya mahali pa kazi.

- Kufanya makongamano ya wataalam wa masuala ya Usalama na Afya mahali pa kazi.

- Kuandaa maonesho yanayolenga katika kubadilishana uzoefu wa uzingatiaji wa usalama na afya katika sehemu mbalimbali za kazi.

- kutoa tuzo kwa waajiri wanaozingatia vyema viwango vya usalama na afya, ambao leo hii Mheshimiwa Mgeni Rasmi, utawakabidhi tuzo zao hapa.

Katika shughuli tajwa, takribani maeneo ya kazi 80 yameshiriki katika maonesho ambapo kumekuwa na mwitikio mkubwa ukilinganisha na mwaka jana ambapo maeneo ya kazi 35 tu ndiyo yaliyoshiriki. Aidha, kwa mwaka huu washiriki 32, wameshiriki katika tuzo ikilingalishwa na washiriki 17 wa mwaka jana.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi; kubwa zaidi katika maadhimisho haya, ni mafanikio tuliyoyapata katika utekelezaji wa mkakati wa sasa wa Taasisi yetu wa kuhakikisha kuwa tunaifikia sekta isiyo rasmi ambapo kwa mwaka huu tumetoa mafunzo ya Usalama na Afya katika sekta za madini, misitu,

viwanda vidogo, elimu na biashara ndogo ndogo ambapo jumla ya wajasiriamali wadogo wapatao 3,672, katika maeneo mbalimbali ya Kanda za Kaskazini, Kanda ya Ziwa, Kanda ya Kusini na pamoja na Nyanda za Juu Kusini walifikiwa hususan mikoa ya Songwe, Lindi (maeneo ya Namungo), Geita, Dar es Salaam. Kwa hapa Dodoma jumla ya wajasiriamali wenye viwanda vidogo na biashara ndogo ndogo wapatao 1,200, waliweza kupata mafunzo hayo. Vilevile, OSHA imetoa mafunzo kwa madaktari kutoka hospitali mbali mbali nchini wapatao 80. Mafunzo haya yalijikita katika kuangazia umuhimu wa utoaji wa taarifa za magonjwa na ajali wanazozipokea katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi; pamoja na makundi hayo tuliyoyafikia kundi ambalo tumelitazama pia kwa jicho la pekee ni watu wenye ulemavu ambao wakati mwingine huwa wanasahaulika katika masuala mbalimbali ikiwemo Usalama na Afya mahali pa kazi. Hivyo sisi kama OSHA tumefanya mafunzo maalum kwa ajili ya watu wenye ulemavu wapatao 300 wanaojihusisha na shughuli mbali mbali ya uzalishaji mali. Mafunzo haya tuliyatoa kwa kuzingatia ukweli kwamba watu wenye ulemavu wanauwezo wa kufanya kazi aidha kwa kujiajiri ama kuajiriwa ambapo pamoja na mafunzo hayo walipatiwa vifaa vya kujikinga na vihatarishi ili kuwawezesha kufanya kazi zao katika hali ya usalama na afya.

Mafunzo hayo yote kwa makundi tajwa yamegharamiwa na Serikali.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi, hakuna shaka sote tunatambua kwamba mwelekeo wa nchi yetu kwa sasa ni kujenga mazingira mazuri ya uwekezaji, na hivyo katika kuelekea huko ajira nyingi zitazalishwa na watanzania wengi wataajiriwa katika sekta mbalimbali za uzalishaji. Ni dhahiri kwamba maendeleo haya kiuchumi yataambatana na athari mbalimbali za kiusalama na kiafya, ambazo kama hakuna mkakati madhubuti wa kuzuia athari hizo, nguvu kazi ya taifa itakuwa hatarini. Hivyo, OSHA kama Taasisi yenye dhamana ya kusimamia masuala ya Usalama na Afya imejipanga vyema kuhakikisha kuwa athari hizo zinadhibitiwa.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi; kwa kuhitimisha ningependa kuwakumbusha waajiri, wafanyakazi na umma kwa ujumla kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia viwango vya usalama na afya vilivyowekwa na serikali kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi; ningependa kutumia fursa hii kuushukuru uongozi wa Mkoa wa Dodoma ukiongozwa na **Comrade Antony Mtaka** kwa ushirikiano waliotupatia sambamba na kukubali kuwa mwenyeji wa maadhimisho haya. Ni matumanini yangu kuwa imekuwa ni fursa nzuri kwa wakazi wa Jiji la Dodoma kufanya biashara na kujifunza kutoka kwa washiriki waliotoka katika mikoa mbalimbali nchini kuhusiana na utekelezaji wa Sheria ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi.

Baada ya taarifa hii ya maadhimisho ya mwaka huu Mheshimiwa Mgeni Rasmi, naomba nikushukuru tena wewe binafsi na viongozi wote uliombatana nao. Aidha, shukrani hizi pia ziwaendee wadau wetu na washiriki wote wa maadhimisho haya.

Kwa niaba ya menejimenti nzima ya OSHA, tunapenda kuwawatakia maadhimisho mema.

Asanteni kwa kunisikiliza